# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE

# MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI CHA TAREHE 18.10.2021

Oktoba, 2021

## MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI CHA TAREHE 18.10.2021

### AGENDA. NA. BHDC/CMT/MUHT. 1.10.2021 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 02:20 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe.

### AGENDA. NA. BHDC/CMT/MUHT. 2.10.2021 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 11.10.2021

Kuhusu uchimbaji wa madini katika Kata ya Bukuba na Janda iliagizwa, taarifa ya uchimbaji wa madini hayo, itolewe kwa Mh. Mkuu wa Wilaya na Katibu Tawala Mkoa.

Agizo lilizingatiwa, barua kwa Katibu Tawala Mkoa ilishawasilishwa bado kwa Mh. Mkuu wa Wilaya.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuagiza taarifa ya Uchimbaji wa Madini kata za Bukuba na Janda iliwasilishwe kikao kijacho pamoja na barua ya kwa Mh. Mkuu wa Wilaya.

Kuhusu fedha ambazo Afisa Ugani wa kata ya Muyama anazo kiasi cha zaidi ya Tsh. 3,000,000/= iliagizwa fedha hizo zipelekwe bank.

Agizo halikutekelezwa kwani, Afisa Ugani huyo yupo likizo.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea na kuagiza, ufanyike utaratibu wa Afisa Ugani huyo, kuweka fedha benki hata kama yupo likizo.

Kuhusu utoaji wa leseni za biashara kwa wafanyabiashara wa Wilaya ya Buhuigwe, iliagizwa orodha ya wafanyabiashara hao iandaliwe.

Agizo halikutekelezwa, uandaaji wa orodha hiyo utafanyika baada ya wiki mbili hadi Maofisa biashara waende kuwatembelea wafanyabiashara hao Vijijini.

Kuhusu Sheria na adhabu ya kosa la utoro kazini, iliagizwa iandikwe kwa Lugha nyepesi na kugawa kwa Wakuu wa Idara na Vitengo ili waweze kuwaeleza/ kuwapatia wasaidizi wao. Kwa upande wa idara za Elumu ya Msingi na Sekondari wapewe walimu Wakuu na Wakuu wa shule ili wabandike kwenye mbao za matangazo Shuleni.

Agizo halikutekelezwa kwani, utaratibu bado unafanyika kwa kufanya mawasiliano na ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ili kuweka sawa kwa upande wa Watumishi wa Kada ya Elimu.

Kuhusu maboma ya vyumba vya madarasa ya Sekondari, iliagizwa idara ikaandae tena na kuwasilisha ikionesha hatua iliyofikia kwa kila moja.

Agizo lilitekelezwa, orodha ya maboma iliwasilishwa hatua iliyofikiwa kwa kila boma.

Zaidi ya hayo, ilitolewa taarifa kuwa kuna upungufu wa vyumba 26 vya madarasa hata hivyo, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vymba 53 vya madarasa kwa idadi tofauti kwa shule zote za Serikali ambapo ujenzi ukikamiliaka utakuwa umeondoa changamoto ya upungufu huo.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kuagiza maandalizi yafuatayo ya awali yaanze,

1. Uundaji wa Kamati (kamati ya Ujenzi, Manunuzi na Mapokezi).
2. Kujiridhisha uhalali wa maeneo ya ujenzi huo.
3. Vifaa vya ujenzi kama vile tofali na mawe.
4. Ramani pamoja na Makadilio ya Gharama ya Halmashauri (Council Estimate).
5. Bati na vifaa vingine vinunuliwe kwa pamoja kwa vyumba vyote 53.

Kuhusu Mafundi ilielezwa kuwa wameagizwa watumie "**Single Sourse**" hivyo Wakuu wa shule wataelezwa kuwasilisha majina ya mafundi kutoka katika maeneo yao.

Baada ya maelezo hayo, Mkurugenzi alishauri, Mafundi wawe wazuri wenye uzoefu ili majengo yawe na ubora unaotakiwa.

Aidha iliundwa Kamati ya ufuatiliaji na Walezi wa kila Shule kama ifuatavyo,

A). KAMTI YA UFUATILIAJI.

1. Lissa Shirima
2. Mussa Ilanda
3. Jerry Mwakapemba
4. Deogaratius Chubwa
5. Joel Mtabwa
6. Dr. Themistocles Kamugisha
7. Christopher Kajange
8. Nice Msuya
9. Fortunatus Mgimba
10. CPA Suphian Juma

**B) WALEZI WA SHULE**

1. **Buyenzi Sekondari-** Issack Masenya
2. **Bwafumba Sekondari –** Makisio Maganga
3. **Janda Sekondari** - Noel Kasaya
4. **Nyamilambo Sekondari-** Pius Ndijuye
5. **Kibande Sekondari-** Weisy Wikedzi
6. **Kibwigwa Sekondari** - Emma Malilo
7. **Yanza Sekondari** - Charles Mabuga
8. **Mkoza Sekondari** - Alphonce Haule
9. **Nyakimue Sekondari** - Masau Koligo

10. **Mkatanga Sekondari** - Fredick Kanyondwi
11. **Muharulo Sekondari** - Fredy Fandey
12. **Muhinda Sekondari** - Hamenyimana Mbonabucha
13. **Nyaruboza Sekondari** - Christopher Kajange
14. **Munanila Sekondari** - Marycelina Mbehoma
15. **Kahunga Sekondari** - Angelo Kalolo
16. **Munzeze Sekondari** - Alex Nkamata
17. **Muyama Sekondari** - Mussa Ilanda
18. **Manyovu Sekondari** - Deogratius Chubwa
19. **Buha Sekondari** - Khalfan Bwangalo
20. **Rusaba Sekondari** - Idrissa Naumanga

Aidha iliagizwa vikao vya Kamati za Maendeleo ya Kata (WODC) vifanyike haraka siku ya Alhamis na Ijumaa tarehe 21-22/10/2021 na walezi hao wa shule wahudhurie na wawaeleze kuanza kufanya maandalizi ya awali kwa ajili ya ujenzi huo.

**AGENDA. NA. BHDC/FUM/MUHT. 9.11.2021. MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO.**

Idara ya fedha na biashara, iliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha Tsh. 1,910,000,000.00 kwa Mchanganuo ufuatao;

1. Fedha za UVIKO zitatumika kutekelezamiradi ifuatayo,
   - Vyumba 53 vya madarasa ya sekondari Tsh. 1,060,000,000.00
   - Vyumba 2 shule shikizi Tsh. 40,000,000.00
   - Ununuzi wa X-RAY Tsh. 420,000,000.00
   - Nymba za watumishi Hospitali ya Wilaya Tsh. 90,000,000.00 na
   - Jengo la dharura Hospitali ya Wilaya Tsh. 300,000,000.00
2. Kupitia tozo ya Miamala.
   - Bweni la Wanafunzi wenye mahitaji maalum Tsh. 80,000,000.00
   - Ujenzi wa vyumba vya madarasa 15 shule za sekondari Tsh. 187,500,000/=
3. Vyanzo vingine.
   - Ujenzi wa vyoo na miundombinu ya maji katika vituo vya kutolea huduma 12 Tsh. 698,158,000.00
   - Uimarishaji wa huduma ya uhai na ulinzi wa mama na mtoto Tsh. 7,881,150

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili kuridhia na kukubaliana kutekeleza miradi hiyo kwa kuzigatia mlongozo iliyotolewa na kuikamilisha kwa muda ulipangwa.

**AGENDA. NA. BHDC/CMT/MUHT.4.10.2021 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**

- **UJENZI WA SOKO MUYAMA**

Ilitolewa taarifa kuwa Soko la Muyama linatakiwa kukabidhiwa tarehe 2.11.2021, hivyo vibanda 350 vinatakiwa kujengwa na wananchi kuzunguka soko hilo.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea, kujadilidi kuridhia na kuagiza;

- Idara ya Ujenzi iandae Michoro ya vibanda hivyo.
- Vibanda vijengwe na wananchi kwa maelekezo ya Halmashauri.
- Halmashauri ya Kijiji ishirikishwe, Muhtasari wa Makubaliano uwasilishwe kwenye kikao kijacho.

- **MITI YA MISINDANO**

Miti aina ya Misindano 1,060,000 iliandaliwa katika Kijiji cha Kajana, na baada ya kugawa kwa wananchi walioomba imebaki 500,000.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea, kujadili, kuridhia na kushauri, Shule zipewe taarifa ili ziweze kutuma maombi na kupanda kwenye mipika ya meneo ya shule ili kuzuia uvamizi.

Pamoja na hayo ilielezwa kuwa miti mingine itapandwa kwenye eneo la Halmashauri Bwega na Bukuba.

- **UJENZI WA NYUMBA ZA WAKUU WA IDARA**

Kuhusu ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Idara, iliagizwa Mhandisi wa Kilimo (**Mjairi B. Julius**) na Mhandisi wa Ujenzi (**Jerry Mwakapemba**) waandae ramani na kuwasilisha kwenye Kikao.

- **TAARIFA YA MIRADI.**

Ilitolewa taarifa kuwa idara ziwasilishe maombi ya Miradi Ofisi ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji mwisho tarehe 30.10.2021 kwa ajili ya kuungalisha na kuwasilisha TAMISEMI.

- **WATUMISHI WAGENI**

Walitambulishwa na kukaribishwa Watumishi wageni wafuatao,

1. Alawi Omari (Mhandisi Ujenzi)
2. Juma Kasambiko (SLO Idara ya Elimu Sekondari)

**AGENDA. NA. BHDC/CMT/MUHT. 4.10.2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 04:34 asubuhi kwa kushukuru wajumbe kuhudhuria kikao.

**MUHTASARI HUU WA KIKAO CHA SALA YA ASUBUHI UMESAINIWA NA;**

| | |
|---|---|
| JINA KAMILI SAMWEL ELSON | JINA KAMILI MASAU M. KOLIGO |
| SAINI........ | SAINI........ |
| TAREHE 25/10/2022 | TAREHE 25/10/2022 |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

AFISA UTUMISHI NA UTAWALA BUHIGWE

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE